

Marekebisha yanayopendekezwa ya *Kitabu kya Adabu*

¶4

Numero ya Ombi: 20980-GA-¶4-C; Bard, David - Lansing, MI, Etats-Unis wa Baraza ya Maaskofu.

Utangulizi Mupya ya Chapitre ya 4

Kanisa Methodiste Unie iko structure ya uunganisho yenye inadumishiwa kupitia msururu wake wa mikutano.

Kanisa Methodiste Unie iko kanisa yenye inaunganishiwa, mutandao ya makutano, mikutano na ma agence yeenye iliunganishiwa kupitia urithi wabo, ma valeur, kanuni na mission yabo moya, juu kwa pamoya kubafanya banafunzi ba Yesu Kristo ku babadiliko ya dunia.

Kanisa Methodiste Unie imepangiwa katika mikutano inne ya kuunganisha.

1. Konferensi Kuu ni chombo cha kutunga sheria cha kimataifa cha Kanisa Methodiste Unie yenye ilikabidhiwa mamulaka ya kutunga sheria kwa mambo yote yenye inahusiana waziwazi kabla ya Mungu wa Butatu kutambua njia ya Mungu kwa juu ya kanisa.

2. Mikutano za Centrale na za Mamulaka ziko na jukumu ya kubachagula na kubateula maaskofu wa Kanisa Methodiste Unie. Kwa kuongezeya, mikutano za Centrale zimepatiwa bahati ya adapter Kitabu Kya Discipline kulingana na ma contexte yabo ya kipekee.

3. Mikutano za Kila Mwaka ziko na jukumu ya kupanga bashirika na viongozi wa dini kutekeleza mission ya Kanisa Methodiste Unie ndani ya eneo yabo.

4. Mikutano ya Charge/Kanisa ziko jukumu ya kupanga makutano kwa juu ya mission na huduma katika communaute yake.

Ingawa Kanisa Methodiste Unie ina uhusiano katika nature, na inashiriki kanuni moya, kila moya ya mashirika imepangwa kama mashirika ya unique yenye inatawaliwa na mikutano. Bajumbe wa Mukutano Mukubwa kutoka kote mu ulimwengu banajumuisha kusanyiko ya batu mbalimbali na benye karama za kipekee benye balikusanyika juu ya kutekeleza kwa pamoya buongozi kupitia Mukutano ya Kikristu. Kusudi ya Mukutano Mukubwa iko kuhakikisha kwamba uunganisho inabakiya kuwa kweli kwa wito wake, ukizingatia kile ambakyo Kristo anafanya mu dunia na kufanya bupya na kukuza kujitolea kwetu kushiriki katika mission ya Mungu.

Kihistoria, Mukutano ya Kimethodiste ilianza wakati John Wesley alipoalika nombre ndogo ya bahubiri katika uhusiano kuungana naye katika kutambua mapenzi ya Mungu kwa juu ya mouvement. Balitumiya buzoefu kutoka kwa ma classe na ma groupes zabo kwa madhumuni ya kubasaidiya bashiriki kukua katika uhusiano wabo na Yesu Kristo na katika kutembea kwabo pamoya naye. Kanuni za msingi za kuongoza kuwa ndani ya mikutano zilitegemea maswali kutoka kwa ma cours lakini zilitumika kwa kazi ya bahubiri: Nini kufundisha? Ginsi ya kufundisha? Nini ya kufanya? Kwa iyi njia balishughulikiya contenu, méthode na ma stratégie. Kuwa ndani ya mikutano katika Kanisa Meth-

odiste Unie imekuya kufahamisha maisha katika kila nivo, yenye inafanya kazi (1) kuhuisha na kuunda utawala, (2) kuhuisha na 'kutiya adabu' mikusanyiko yote ya bale benye banadai jina ya Methodiste, na (3) kutiya moyo huduma ya uinjilisti kwa bale benye banahitaji Injili ya kila kabila, taifa na rangi. Izi Matendo tatu ya kimsingi katika lugha ya kimadhehebu zaidi inajumuisha kanuni, umoja na uamsho.

Kanuni zile zile zinatumiwa katika kila mukutano ya malipo, kila mwaka wa mukutano, ya kimamulaka na mukutano centrale, na kila baada ya miaka inne katika nivo ya dunia nzima kama Mukutano wa Kila Mwaka.

Mutazamo:

Utangulizi yenye ilirekebishiwa inatoa theolojia ya kina zaidi ya mikutano.

¶701

Numero ya Ombi: 21074-GA-¶701; Arroyo, Giovanni - Washington, DC, Etats-Unis kwa Commission Mukubwa juu ya Dini na Rangi.

Majina za Banachama Itafanywa publique

Ongeze Paragraphe 701:

Ili kuhakikisha utofauti na uwazi, jina na taarifa husika za idadi ya watu (kama vile uhusiano wa kanisa, jinsia, kabila, na ulemavu (kama zipo)), za batu bote benye balichaguwa kuhudumu kwenye kikosi kazi ao kamati ya dharura ambayo kazi yabo ina impacter dini kwa ujumla wake litafichuliwa hazarani. Baada ya maombi, taarifa kama zilezitatolewa kwa maandishi kwa GCORR na GCSRW. Bufichuzi wa hadharani wa habari hii utafanywa wakati wa uteuzi, kupitiya buchapishaji yenye inafaa, buchapishaji kwenye tovuti zinazohusika, na kwa njia nyingine ngixi inafaa. Vile vile, ikiwa nafasi itajazwa, bufichuzi itafanywa mara mora sana.

Mutazamo:

Byombo bya Kanisa, ikiwa ni pamoya na Baraza ya Maaskofu, wakati mwingine ilichaguliwa bikosi bya kazi na kamati za zarura zenye impact ya ndani na ya kimataifa. Michakato ya buteuzi ya haki na ya uwazi ina akisi butofauti wa dini ni muhimu juu ya kusaidiya kuhakikisha ushiriki muzuri katika kazi ya haki na takatifu ambayo husababisha maamuzi, mapendekezo na vitendo vinavyoaminika.

¶717

Numero ya Ombi: 20981-GA-¶717; Wharff, Mark -